

Co-operative Development in Tanzania, Recession and the Way Forward
Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Tumekwama Wapi na Tunasongaje Mbele

**Wasilisho hili, liliwasilishwa katika kongamano la Majilisi ya Sita ya Chuo Kikuu Cha
Ushirika Moshi, Tarehe 2, December, 2020**

Gratian Cronery Rwekaza (Mhadhiri)

Idara ya Menejiment Kitivo cha Biashara na Sayansi za Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi

Christina M Maeda (Mhadhiri Msaidizi)

Idara ya Menejiment Kitivo cha Biashara na Sayansi za Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi

Muhimu

Andiko hili limelenga kujenga uelewa wa ushirika kama falsafa, misingi na ueneaji wake nchini Tanzania. Pia kujenga uelewa wa ushirika kwa ujumla wake ambao umekuwa ukikumbwa na vikwazo na majanga ili kuona nii kifanyike katika kuleta ukombozi wa ukuaji wa ushirika nhini Tanzania. Msomaji, msikilizaji na mtumiaji hana budi kujua kwamba, andiko hili halilengi kujenga uchochezi bali kuleta uelewa. Pia yaliyomo humu ndani ni matokeo ya uzoefu na udadisi wa mwandishi. Andiko hili lisitumiwe tofauti na mantiki na makusudio ya kujenga uelewa na kuibua majadiliano ndani ya kongamano na kwa mtumiaji wa hapo badae.